

Imetolewa tarehe: 13 Januari, 2012

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

MKUTANO WA WAMILIKI WA MADUKA YA DAWA BARIDI MKOANI DAR ES SALAAM TAREHE 17 JANUARI 2012

1. Utangulizi

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) inatekeleza Mpango wa kuboresha Maduka ya Dawa Baridi (DLDB) kuwa Maduka ya Dawa Muhimu (DLDM). Mpango huu unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma bora za dawa kwa wananchi hususan waishio katika maeneo ya miji midogo na vijijini.

TFDA kwa kushirikiana na Manispaa za Kinondoni, Temeke na Ilala, wameandaa mkutano wa wamiliki wa Maduka ya Dawa Baridi mkoa wa Dar es Salaam kuhusu uendeshaji wa mafunzo ya wamiliki na watoa dawa wa Maduka ya Dawa Muhimu ikiwa ni hatua mojawapo ya utekelezaji wa Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu.

2. Walengwa

Walengwa ni wamiliki wa Maduka ya Dawa Baridi mkoani Dar es Salaam ambao maduka yao yalifanyiwa ukaguzi wa awali na kupewa maelekezo ya kufanya marekebisho ili kukidhi vigezo vya Maduka ya Dawa Muhimu.

3. Mahali na muda

Ukumbi wa PTA katika viwanja vya Maonesho vya Mwalimu J. K. Nyerere, Saba saba tarehe 17 Januari 2012 kuanzia saa 2.30 hadi 5.00 asubuhi.

Imetolewa na

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA),
Barabara ya Mandela, External- Mabibo,
S.L.P 77150,

Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: +255 22 2450512 / 2450751 / 2452108

Nukushi: +255 22 2450793,

Barua pepe: info@tfda.or.tz

Tovuti: www.tfda.or.tz